

# Kupotea kwa Maneno Chanzi katika Lahaja za Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Lahaja ya Kipemba

Sauda Uba Juma

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Tanzania

## Uwasilishaji wa Makala

Kupokelewa: 2025-01-04

Kurekebisha: 2025-04-15

Kukubaliwa: 2025-04-19

Kuchapishwa: 2025-04-20

## Maneno Muhimu

Bayana

Chanzi

Kategoria

Usanifishaji

## Jinsi ya Kurejelea Makala:

Juma, S. U. (2025). Kupotea kwa Maneno Chanzi katika Lahaja za Kiswahili: Uchunguzi Kifani wa Lahaja ya Kipemba. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, 3(1), 37-46.

## Ikisiri

Tafiti mbalimbali zinaonesha kwamba, baadhi ya lahaja za Kiswahili zinaelekea kupoteza uasili wake kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za kijamii na kihistoria. Kupotea kwa maneno chanzi katika lahaja ni tatizo linalohitaji umakini wa haraka kwa sababu huenda kizazi kijacho kisiweze kuyatambua kabisa maneno hayo. Pamoja na ukweli huo, hakujawa na uchunguzi wa kina unaoonesha mifano kuntu ya maneno chanzi ambayo yanaonekana kupotea katika lahaja mbalimbali za Kiswahili ikiwamo lahaja ya Kipemba. Hivyo, makala hii inachunguza mifano ya maneno chanzi yanayoanza kupotea katika lahaja hiyo. Kwa hakika uchunguzi huu utasaidia kuyaweka bayana maneno hayo ili yabaki hai na yaendele kutumiwa na watafiti pamoja na waandishi mbalimbali wa lugha ya Kiswahili na lahaja zake. Aidha, makala imechunguza sababu pamoja na athari za kupotea kwa maneno chanzi. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Umuundo iliyoasisiwa na De Saussure mwanzoni mwa karne ya 20. Data za makala hii zimekusanywa kupitia mbinu ya usomaji wa nyaraka, ushuhudijaji, usaili na hojaji. Makala imebaini kuwa kuna maneno chanzi mbalimbali ambayo yamepotea na mengine yanaendelea kupotea katika lahaja hiyo. Aidha, makala inatoa mchango mkubwa kwa taasisi za BAKITA na BAKIZA kwa kuwa zitaweza kuyatumia maneno hayo katika uundaji na usanifishaji wa istilahi za Kiswahili. Pia, watafiti na waandishi mbalimbali wa lahaja za Kiswahili wataweza kuyatumia maneno hayo katika tafiti zao. Makala imetoa mapendekezo ya kufanyika kwa uchunguzi zaidi wa maneno hayo katika lahaja nyingine mbalimbali za Kiswahili.

Copyright © 2025



## Utangulizi

Lugha na lahaja si vitu vilivyo tuli bali huweza hubadilika. Kila lahaja ina sifa zake za kipekee lakini pia inashiriki katika mabadiliko haya kupitia mwingiliano na lugha nyingine, mabadiliko ya matumizi na mitindo ya mawasiliano. Wataalamu mbalimbali katika fani ya lugha na isimu kama vile Valero-Garces, (2014) na Miller (2021) wanazungumzia mchakato huu kwa kina, wakichunguza sababu zinazochangia mabadiliko haya, athari zake kwenye utamaduni wa jamii na umuhimu wa kuhifadhi lugha za asili. Mtaalamu wa lugha, Ngugi wa Thiong'o (1986), anasisitiza umuhimu wa lugha za asili katika kujenga utambulisho wa kitamaduni. Aidha, anazungumzia jinsi lugha za asili zinavyoweza kudharaulika kutokana na ushawishi wa lugha za kigeni, hasa katika muktadha wa kisasa wa teknolojia. Aidha, anadai kuwa lugha ni zaidi ya chombo cha mawasiliano kwa kuwa ni sehemu ya urithi wa tamaduni zetu. Hii inaonyesha jinsi mabadiliko ya maneno yanavyoweza



kuathiri sio tu muundo wa lugha, bali pia utamaduni wa jamii inayozitumia. Kwa mfano, mabadiliko katika matumizi ya maneno yanaweza kuakisi mabadiliko ya mitazamo na thamani za jamii.

Harrison (2007) amechunguza athari na umuhimu wa kuhifadhi lugha asili ili kuimarisha utambulisho wa kitamaduni. Hata hivyo, wakati maneno na dhana mpya zinapokaribishwa katika lugha ya asili, kuna hatari ya kupoteza urithi wa lugha na tamaduni za zamani. Naye, Crystal (2010) katika utafiti wake aligundua kuwa, mabadiliko ya maneno chanzi yamechochewa na teknolojia na mitandao ya kijamii ambayo inarahisisha mwingiliano wa lugha. Mtafiti huyo anazidi kueleza kwamba katika zama hizi za kidijitali maneno chanzi yanaweza kupotea au kubadilika kwa urahisi na hivyo basi ni muhimu kuyahifadhi. Katika muktadha huu, matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mitandao ya kijamii yameleta athari kubwa katika mabadiliko ya maneno ya asili, kwa kuwa maneno mapya yanaingia kwenye matumizi ya kila siku. Hivyo, kuna hatari ya kupoteza baadhi ya maneno hayo. Vilevile, Mekacha (2011) anaeleza kwamba, kuna umuhimu mkubwa wa kuzitumia lugha za kijamii katika mawasiliano ya jamii husika.

Kwa upande wake Ibrahim (2024) alichunguza umuhimu wa lugha za kijamii katika huduma za afya pamoja na athari za kutozingatiwa kwa lugha za kijamii katika kutoa huduma za afya. Mtafiti huyu alirejelea jamiilugha mahususi za Watumbatu na Wakojani katika kisiwa cha Zanzibar. Katika utafiti wake, alibaini kwamba matumizi ya lugha za kijamii yana mchango mkubwa katika kufanikisha mawasiliano baina ya watu wa jamiilugha husika. Kwa ujumla katika sehemu hii, tumejadili kwa ufupi mapitio kuhusu umuhimu wa kutumia lugha za asili kama sehemu ya utangulizi wa makala hii. Sehemu ifuatayo inahusu nadharia iliyoongoza utafiti huu.

### **Nadharia ya Utafiti**

Uchambuzi wa data za makala hii umeogozwa na nadharia ya Umuundo iliyoasisiwa na Ferdinand De Saussure mwanzoni wa karne ya 20. Katika kitabu chake cha *Course in General Linguistics* kilichoandikwa na wanafunzi wake mwaka 1916, De Saussure aliibua na kutofautisha dhana mbalimbali za kiisimu. Mathalani, anazungumzia uchunguzi wa mabadiliko ya lugha ambao unaweza kufanywa kidiakronia au kisinkronia. Kupitia dhana hizo, mtafiti anaweza kubaini mabadiliko mbalimbali yaliyotokea katika lugha kutokana na mpito wa wakati. De Saussure anadai kila msamiati wa lugha una thamani kwa wakati wake na kwa hivyo, neno lina thamani yake ya leo sio kihistoria. Aidha, mwanaumuundo huyo, anazungumzia Mfumo wa Lugha (*langue*) ambapo anaona kwamba, lugha ina mfumo ambao ni jumla ya ishara zilizomo akilini mwa kila mzawa wa lugha mwenye akili timamu. Hivyo, kila lugha ina mfumo unaojitosheleza kisarufi na kimsamiati. Kwa mnasaba huo, hakuna lugha mbili zinazofanana kisarufi na kimsamiati. Hii inatokana na ukweli kwamba, watu wanabuni msamiati kwa kuwa umo katika mazingira yao na hivyo wanahitaji kuurejelea.

Dhana nyingine anayoizungumzia ni Utendaji (*parole*) Kwa mujibu wa De Saussure, utendaji ni usemaji wa mtu binafsi ikiwa ni sehemu ya kanuni na ishara alizonazo akilini mwake. Hivyo, Utendaji unaweza kuathiriwa na kasoro nyingi tofauti na Mfumo wa Lugha ambao uko palepale, lazima kanuni na taratibu za lugha zifuatwe kwa kila mwanajamii-lugha husika. De Saussure anazidi kuisitiza kwamba, ili utafiti wa lugha uwe faafu zaidi lazima uzingatie Mfumo wa Lugha, Utendaji Diakronia na Sinkronia. Hivyo, katika makala hii Nadharia ya Umuundo imekuwa ni faafu zaidi kwa kuwa imemsaidia mtafiti kubaini mabadiliko mbalimbali ya maneno chanzi yaliyopotea kutokana na mpito wa wakati (diakronia). Vilevile, pamoja na kubaini kupotea kwa maneno hayo, bado wanajamii wanaendelea kutumia maneno mapya yaliyobadilika kwa kadri walivyokubaliana kuyatumia. Hata hivyo, maneno mapya yaliyopokelewa katika lahaja hiyo yanaendelea kutumika kwa kufuata kanuni na taratibu za mfumo wao wa lugha kutokana na umilisi walionao kuhusu lahaja yao.



## Methodolojia

Utafiti uliovyaza makala hii ulikuwa ni wa kimaelezo na sio wa kitakwimu kwa kuwa mwegamo wake umezingatia uchambuzi wa data kitaamuli. Mbinu ya usampulishaji lengwa na usampulishaji tajwa ilitumika kupata sampuli ya watoataarifa 40 waliohusishwa katika utafiti huu. Sampuli hiyo ilijumuisha vijana kuanzi miaka 20 hadi 45 ambao walitoa taarifa za maneno yanayotumiwa kwa wakati huu katika Kipemba. Hali kadhalika, wazee wenye umri wa kati ya miaka 50 hadi 80 walitumika kutupatia orodha ya maneno ya asili yaliyopotea katika lahaja hiyo. Wazee hao walihusishwa kutoa taarifa za sababu Vilevile, Uteuzi huo kwa wazee umezingatia kigezo cha umri mkubwa na uwezo wa kuzungumza Kipemba cha asili. Aidha, makala hii ilitumia mbinu zaidi ya moja ili kupata data thabiti ambazo ziliweza kukidhi vema lengo la utafiti huu. Mbinu hizo ni usomaji wa nyaraka maktabani, ushuhudiaji, hojaji na usaili. Mapitio ya machapisho yaliyosomwa, yalimsaidia mtafiti kupata data za maneno yaliyotumika katika uandaaji wa hojaji. Aidha, mbinu ya ushuhudiaji ilitumika kubaini maneno mbalimbali yaliyokuwa yakitumiwa na wanajamii uwandani. Vilevile, mbinu ya usaili iliwahusisha watoataarifa teule wenye umilisi na uwezo wa kutumia maneno chanzi ya Kipemba. Kwa upande wa mbinu ya hojaji mtafiti aliandaa dodoso na kuorodhesha jumla ya maneno 100 yaliyoandaliwa kwa Kiswahili sanifu kupitia mbinu ya udurusu wa nyaraka maktabani. Hivyo, mbinu mchanganyiko zilizotumika zilimsaidia mtafiti kupata data faafu na zenye tija katika kufanikisha lengo la makala hii.

## Mjadala wa Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa kuzingatia kategoria za maneno zilizochunguzwa katika makala hii ambazo ni: nomino, vitenzi na vivumishi pamoja na maneno ya utamaduni. Maneno yote yaliyobainishwa katika makala hii yamepatikana kwa kutumia mbinu ya ushuhudiaji, usaili na hojaji. Hivyo, ili kupata picha kuntu ya tunachokizungumzia, tuchunguze mifano ya kategoria hizo.

## Maneno Chanzi Yaliyomo katika Kategoria ya Nomino

Katika sehemu hii tumechunguza maneno yanahusu kategoria ya nomino za aina mbalimbali. Data inaonesha kwamba baadhi ya nomino hizo zimeanza kupoteza uasili wake. Jedwali Na. 1 lifuatalo linathibitisa hayo.

Jedwali na. 1: Maneno Chanzi Yaliyomo katika Kategoria ya Nomino

Na.	Maana ya Asili	Maana Iliyobadilika	Tafsiri ya Kiswahili
1.	<i>Shengeremu</i>	<i>Hamu</i>	Hamu
2.	<i>Viteweji</i>	<i>Vitimbi</i>	Visa
3.	<i>Kisuunzi</i>	<i>Kizunguzungu</i>	Kizunguzungu
4.	<i>Jeleza</i>	<i>Kichefuchefu</i>	Kichefuchefu
5.	<i>Mwase/mwasada</i>	<i>Njaa</i>	Njaa
6.	<i>Sitalimu</i>	<i>Kua/baleghe</i>	Baleghe
7.	<i>Kidusi</i>	<i>Kivundo</i>	Harufu mbaya
8.	<i>Kisukusuku</i>	<i>Kisugudi</i>	Kiwiko
9.	<i>Kati</i>	<i>Kyumba</i>	Chumba
10.	<i>Muye</i>	<i>Nvuke</i>	Mvuke

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2024)

Katika makala hii matokeo yameonesha kwamba kuna maneno chanzi mbalimbali ambayo yameanza kupotea katika Kipemba. Baadhi ya maneno hayo, kwa wakati huu hayajulikani kabisa kwa baadhi ya wanajamii. Hii ni kwa sababu ni nadra sana kwa wanajamii lugha walio wengi, hasa vijana, kuyatumia katika mazungumzo yao ya kila siku. Hivyo, maneno hayo chanzi, yanajulikana kupitia



tafiti kama hizi za kitaalamu kwa watoataarifa ambao ni wazee. Tukichunguza data iliyomo katika Jedwali Na. 1 hapo juu, tunabaini kuwa karibu maneno yote 10 yanaelekea kupoteza uasili wake. Tunadiriki kusema hivyo kwa sababu maneno kama *shengeremu (hamu)*, *kisuunzi (kizunguzungu)* na *jelezi (kichefuchefu)* yanaonekana kufanana zaidi na Kiswahili sanifu kuliko Kipemba. Jambo hili linadhihirisha kile kisemwacho kwenye msingi mmojawapo wa nadharia iliyoongoza utafiti huu. Kupotea kwa maneno chanzi ya Kipemba miongoni mwa vijana kunadhihirisha mabadiliko ya lugha kidakronia. Kwa mfano maneno *sitalimu (baleghe)*, *kidusi (harufu mbaya)* na *kati (chumba)*, yamepotea kutokana na mabadiliko ya lugha na mpito wa wakati kihistoria. Inaweza kukisiwa kuwa kupotea kwa maneno haya chanzi ya Kipemba kunatokana na mwingiliano wa lugha ya Kiswahili na Kipemba shuleni. Vijana wanapokwenda shule wanazoea kutumia maneno ya Kiswahili sanifu na hatimaye kuyaacha maneno ya asili ya lahaja yao.

Katika orodha hiyo ya maneno yanayohusu nomino, kuna maneno ambayo yamepoteza uasili wake na ambayo yanaonekana kutofautiana na Kiswahili sanifu. Hata hivyo, maneno hayo yana tofauti ya sauti tu, lakini yanakaribiana kiumbo na yale ya Kiswahili sanifu. Mathalani, maneno *kyumba (chumba)* na *nvuke (mvuke)* yameibuliwa kutoka maneno chanzi *kati (chumba)* na *nvuue (mvuke)*. Mifano hiyo, inajibainisha dhahiri kwamba lugha ya Kiswahili imeathiri vijana kiasi kwamba maneno wanayotumia yanakaribiana zaidi na Kiswahili kuliko Kipemba. Mathalani, neno *kyumba* linakaribiana zaidi na *chumba* la Kiswahili kuliko neno *kati* la Kipemba. Hata hivyo, kwa mujibu wa nadharia ya De Saussure kuhusu mfumo wa lugha (langue) maneno hayo yamejaribu kudumisha muundo wa lugha ya Kipemba kwa kutumia sauti /ky/ katika *kyumba* badala ya sauti /ch/ ya Kiswahili. Mifano mengine ya maneno hayo katika Kipemba ni *kyama (chama)*, *kyuma (chuma)* na *kyungu (chungu)*.

Hivyo kwa kuwa Kipemba ni miongoni mwa lahaja za Kiswahili, bila shaka lugha hizi zinatokana na lugha moja ya asili. Kwa hivyo, ingawa maneno hayo yanaonekana kusigana na yale ya Kiswahili sanifu, kwa lugha zenye asili moja, Anttila (1972), Massamba (2017) na Asimwe (2019) wanadai kuwa maneno hayo yanakubalika kuwa ni aina moja na ambayo hayana tofauti. Hii inatokana na ukweli kwamba, sauti /kj/ katika neno *kyombo (chombo)* ilibadilika kupitia mchakato ya kifololojia wa unyeyushaji hadi kupatikana kwa sauti /č/ kama ilivyo katika neno *chombo*. Halikadhalika, neno *nvuke* katika Kipemba na *mvuke* katika Kiswahili yanakubalika kuwa ni maneno ambayo hayatofautiani, tofauti ya sauti /n/ katika *nvuke* na /m/ katika *mvuke* ni tofauti ndogo tu zinazosababishwa na utengano wa kijiografia. Kwa mantiki hiyo, tunaweza kusema kuwa maneno *kyumba* na *nvuke* ya Kipemba ni sawa na maneno *chumba* na *mvuke* ya Kiswahili sanifu. Pamoja na mabadiliko hayo ya kifonolojia, ni dhahiri kwamba lugha ya Kiswahili imeathiri Kipemba. Hata hivyo, huenda vijana bado wanadumisha muundo wa kifonolojia wa Kipemba kama inavyoelezwa katika Nadharia ya Umuundo kuhusu dhana ya mfumo lugha. Hivyo, maneno kama *nfupi*, *njinga*, *nkate* ya Kipemba, hutamkwa *mfupi*, *mjinga* na *mkate* katika Kiswahili sanifu.

### **Maneno Chanzi katika Yaliyomo katika Kategoria ya Vitenzi**

Maneno chanzi ya lahaja ya Kipemba yanayohusu vitenzi yameanza kufifia katika jamii kama yanayobainishwa katika Jedwali Na. 2 lifuatalo:



Jedwali na. 2: Maneno Chanzi Yaliyomo katika Kategoria ya Vitenzi

Na.	Maana ya Asili	Maana Iliyobadilika	Tafsiri ya Kiswahili
1.	<i>Chengeya/simile</i>	<i>Pisha</i>	Pishe
2.	<i>Jipa</i>	<i>Jidai</i>	Jidai
3.	<i>Gina</i>	<i>Kinai</i>	Kinai
4.	<i>Gida</i>	<i>Chuja</i>	Chuja
5.	<i>Gwiya</i>	<i>Gwiya</i>	Shika
6.	<i>Kufya</i>	<i>Nongwa</i>	Nongwa
7.	<i>Fyasa</i>	<i>Kera</i>	Kera
8.	<i>Fyosoa</i>	<i>Kosoa</i>	Kosoa
9.	<i>Vyaa</i>	<i>Vyaa</i>	Zaa
10.	<i>Usha</i>	<i>Usha</i>	Ondoa

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2024)

Katika Jedwali Na. 2 hapo juu, maneno 7 kati ya 10 yaliyobainishwa, yamepoteza uasili wake. Mathalani, *chengeya/simile* (*pisha*), *jipa* (*jidai*), *gina* (*kinai*), *gida* (*chuja*), *kufya* (*nongwa*), *fyasa* (*kero*) na *fyosoa* (*kosoa*). Kwa sasa maneno hayo, yanatamkwa na kuandikwa sawa kama yalivyo katika Kiswahili sanifu. Maneno ambayo bado yanaonekana kutunza uasili wake katika Jedwali hilo ni matatu tu ambayo ni: *vyaa* (*zaa*), *gwiya* (*shika*) na *usha* (*ondoa*). Hata hivyo, ingawa maneno hayo yanaonekana kutunza uasili wake, baadhi ya wazungumzaji wanaendelea kuyatumia kama yalivyo katika Kiswahili sanifu. Kulingana na maoni ya watoataarifa, maneno hayo ya asili yanatumiwa zaidi na wazee kuliko vijana. Sababu mojawapo iliyobainika ni kwamba, huenda vijana wanaonekana kuathiriwa zaidi na Kiswahili wakilinganishwa na wazee. Hivyo, katika mazungumzo yao ya kila siku wanajamii wanatumia vitenzi ambavyo havitofautiani sana na vile viliyosanifishwa.

**Maneno Chanzi Yaliyomo katika Kategoria ya Vivumishi**

Mifano mengine ya maneno chanzi ambayo yanaelekea kupotea ni yale yanahusu kategoria ya vivumishi Tuangalie mifano hiyo katika Jedwali lifuatayo hapa chini:

Jedwali na. 3: Maneno Chanzi Yaliyomo katika Kategoria ya Vivumishi

Na.	Maana ya Asili	Maana Iliyobadilika	Tafsiri ya Kiswahili
1.	<i>Tofya</i>	<i>Legevu</i>	Legevu
2.	<i>Ntikati</i>	<i>Ntisatisa</i>	-Siyoiwa vizuri
3.	<i>Kwekwe</i>	<i>Nkondefu</i>	Mwembamba
4.	<i>Mpuchu</i>	<i>Mwepesi</i>	Mwepesi
5.	<i>Kimumuzimumuzi</i>	<i>Kimyakimya</i>	Kimyakimya
6.	<i>-Zondo</i>	<i>Kata</i>	-Vivu
7.	<i>Ng'wafung'wafu</i>	<i>Kwapire</i>	Mlafi
8.	<i>Korovya</i>	<i>Nbaya</i>	Mbaya
9.	<i>Dutumi</i>	<i>Nfupi</i>	Mfupi
10.	<i>-Fyefye</i>	<i>Dhaifu</i>	Dhaifu

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2024)

Katika kategoria ya vivumishi, maneno yaliyopotea yanajitokeza katika hali mbili: kwanza kuna maneno ya asili ambayo yamepotea kabisa na hayatumiki tena. Hata hivyo, kuna maneno mapya yanayotumika badala ya yale ya asili ambayo hayafanani na Kiswahili. Kwa mfano, maneno kama *ntisatisa* (*isiyoiva vizuri*), *nkondefu* (*mwembamba*), *kata* (*mvivu*) na *kwapire* (*mlafi*) yameibuliwa badala ya maneno chanzi *tofya* (*legevu*), *ntikati* (*isiyoiva vizuri*), *zondo* (*mvivu*) na *ng'wafung'wafu* (*mlafi*). Hivyo, kwa mujibu wa misingi ya Nadharia iliyouongoza utafiti huu bila shaka mabadiliko ya maneno hayo,



yamechanuzwa na mabadiliko ya lugha kihistoria. Hali hii inatokana na ukweli kwamba lugha si tuli huwa inabadilika kulingana na mabadiliko ya jamii. Pili, kuna maneno ambayo ingawa yameibuliwa badala ya maneno ya asili, yanaonekana kufanana kiumbo na Kiswahili. Mathalani, maneno *kimyakimya*, *dhaifu* na *mwepesi* ya Kipemba yameathiriwa na Kiswahili kutokana na elimu ya shule wanayoipata vijana. Hivyo, baadhi ya vijana hao huona fahari kutumia vivumishi vya Kiswahili kuliko kutumia vya lahaja yao ya asili. Aidha, maneno *nbaya* (*mbaya*) na *mfupi* (*mfupi*), kutoka maneno asili *korovya* na *dutumi* yanaonekana kuathiriwa na Kiswahili kutokana na mwingiliano wa lugha. Hata hivyo, kwa mujibu wa msingi wa mfumo lugha katika nadharia ya Umuundo maneno hayo yamedumisha muundo wa kifonolojia wa Kipemba.

### Maneno Chanzi Yaliyomo katika Uga wa Kitamaduni

Katika utafiti huu, imebainika pia kuwa kuna maneno asili katika lahaja ya Kipemba kwenye uwanja wa utamaduni ambayo yanaanza kupotea katika jamii ya leo. Maneno yanayohusu utamaduni yamegawanywa katika makundi mawili. Kundi la kwanza linahusu maneno yanayotaja vyakula anuwai vya asili. Kundi la pili, linahusu maneno chanzi yanayogusa mavazi ya aina mbalimbali. Tuchunguze mifano ya maneno yanayohusu vyakula katika Jedwali Na. 4 lifuatalo:

Jedwali na. 4: Maneno Chanzi Yanayohusu Vyakula

Na.	Neno la Asili	Neno Lililobadilika	Tafsiri ya Kiswahili
1.	<i>Mwengo</i>	<i>Supu</i>	supu
2.	<i>Kulfi</i>	<i>Malai</i>	iskrimu
3.	<i>Dona</i>	<i>Sembe</i>	sembe
4.	<i>Hamuri</i>	<i>Andazi</i>	andazi
5.	<i>Nsambwija</i>	<i>Muhogo na ndizi</i>	muhogo wa kuchanganya na ndizi
6.	<i>Nkoba</i>	<i>Ufuta</i>	urorojo unaopatikana katika aina maalumu ya vyakula
7.	<i>Maovu</i>	<i>Mabivu</i>	maziwa yaliyoiva
8.	<i>Ndaza</i>	<i>Chicha</i>	chicha
9.	<i>Ubweche</i>	<i>Wali</i>	wali
10.	<i>Vitobweshwa</i>	<i>Vipopoo</i>	vipopoo

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2024)

Maneno katika Jedwali Na. 4 hapo juu, yanataja vyakula vya aina tofauti. Katika kundi hili, tunabaini maneno kama *mwengo* (supu), *kulfi* (iskrimu), *nkoba* (urojorojo unaopatikana katika aina maalumu ya vyakula) na *hamuri* (andazi) ambayo kwa kiasi kikubwa yamepoteza uasili wake katika matumizi ya jamii ya leo. Hata hivyo, kupotea kwa maneno hayo, kumesababisha kuibuka kwa maneno mengine tofauti na maneno ambayo yalikuwa yakitumika hapo kabla katika Kipemba. Maneno yanayotumiwa kwa sasa badala ya yale chanzi ni *supu* (supu), *malai* (iskrimu), *ufuta* (urojorojo) na *andazi* (andazi). Kupotea kwa maneno hayo, kumesababishwa na kuhamahama kwa Wapemba kwa ajili ya kutafuta maisha bora zaidi. Baadhi ya Wapemba wana desturi ya kusafiri na kuhamia maeneo ya mjini hasa Unguja na Dar es Salaam. Hivyo, uhamaji huu unaathiri baadhi ya maneno ya asili ya Kipemba. Kwa mfano, maneno *supu* (supu), *ufuta* (urojorojo) na *andazi* (andazi) yameathiriwa na Kimjini cha Unguja na Dar es Salaam. Kwa upande wa neno *malai* (iskrimu) ambalo liliibuliwa badala ya neno la asili *kulfi*, limepatikana baada ya kuondoka kwa Muhindi aliyeitwa Kulfi. Kulfi alikuwa maarufu kwa kutengeneza *iskrimu* katika eneo mahususi kisiwani Pemba. Kwa mantiki hiyo, mabadiliko ya kisinkronia na kidiakronia yamesababisha kupotea kwa neno hilo la asili.

Baadhi ya maneno chanzi yaliyopotea katika Kipemba, yamezalisha maneno mengine yenye mwelekeo wa kulandana na Kiswahili sanifu. Mathalani, *dona* (sembe), *nsambwija* (muhogo uliochanganywa na ndizi), *maovu* (mabivu), *ndaza* (chicha), *ubweche* (wali) na *vitobweshwa* (vipopoo). Maneno



hayo ingawa ndiyo yalikuwa chanzi katika Kipemba kwa wakati huu, hayatumiki kwa jamii pana kama inavyostahiki. Maneno yanayotumiwa kwa kiasi kikubwa ni *sembe*, *muhogo wa kuchanganya ndizi*, *mabivu*, *chicha*, *wali* na *vipopoo* ambayo yana mwonekano sawa wa kiumbo na kimatumizi na yale ya Kiswahili sanifu. Lahaja ya Kipemba imeathiriwa sana na Kiswahili sanifu katika kutaja baadhi ya vyakula. Pia Kipemba kimeathiriwa na kuhamahama, mwingiliano wa watu pamoja na mabadiliko ya kihistoria yaliyoikumba jamiilugha hiyo. Mambo haya yamesabisha kupotea kwa msamiati chanzi wa baadhi ya vyakula katika lahaja hii, hivyo kuonesha mabadiliko kidikronia katika jamiilugha hii.

### Maneno Chanzi Yanayohusu Mavazi

Mavazi ni kipengele cha pili cha kitamaduni kilichochunguzwa katika utafiti huu. Jedwali Na. 5 linalofuata linaonesha maneno chanzi ya Kipemba yanayohusiana na mavazi pamoja na mabadiliko yaliyotokea:

Jedwali na. 5: Maneno Chanzi Yanayohusu Vyakula

Na.	Neno la Asili	Neno Lililobadilika	Tafsiri ya Kiswahili
1.	<i>Dege</i>	<i>Kakaniki</i>	Kaniki
2.	<i>Nkuti</i>	<i>Nsuli</i>	Msuli
3.	<i>Mwimba</i>	<i>Nkaja</i>	Kitambaa kinachofungwa tumboni baada ya mama kujifungua
4.	<i>Nfyuo</i>	<i>Suruali ya kamba</i>	Suruali yenye kamba kiunoni
5.	<i>Ubinda<sup>1</sup>/sodo</i>	<i>Nguo za kike</i>	Kitambaa kinachofungwa sehemu za siri
6.	<i>Sigiria/garia ya ng'ombe</i>	<i>Sidiria</i>	sidiria
7.	<i>Mharume</i>	<i>Rubega</i>	Kitambaa kinachowekwa begani na mashekhe
8.	<i>Handawe</i>	<i>Chupi</i>	Chupi
9.	<i>Ulaiti</i>	<i>Sanda</i>	Sanda
10.	<i>Kizoro</i>	<i>Kilemba</i>	Kilemba

**Chanzo:** Data ya Uwandani (2024)

Kutokana na jedwali Na. 5 hapo juu makala hii imebaini yafuatayo: kuna tofauti kubwa ya maneno yanayotumiwa na wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba kwa wakati huu na yale maneno ambayo yalikuwa yakitumiwa kabla ya mabadiliko hayo. Kuna msigano mkubwa baina ya maneno chanzi na maneno mapya yaliyoibuliwa katika lahaja hiyo. Maneno hayo ndiyo ambayo yanayotumiwa na walio wengi hasa vijana katika lahaja ya Kipemba kwa wakati huu. Katika Jedwali hilo, maneno kama *mwimba* (*kitambaa kinachofungwa tumboni baada ya mama kujifungua*), *ubinda* (*kitambaa kinachofungwa sehemu za siri*) na *nfyuo* (*suruali ya kamba*), yanaonekana kupoteza kabisa uasili wake. Hata hivyo, pamoja na kwamba maneno hayo yamepoteza uasili wake kwa sasa, kuna maneno mapya ambayo yameibuliwa na yameshazoeleka kimatumizi kwa wanajamii wake kwa mfano *nkaja*, (*kitambaa kinachofungwa tumboni baada ya mama kujifungua*), *nguo za kike* (*kitambaa kinachofungwa sehemu za siri*) na *suruali ya kamba* (*haina mpira kiunoni*).

Pia, imebainika katika utafiti huu kwamba, baadhi ya maneno yanayohusu mavazi yamepoteza uasili wake kwa kuwa, huenda nguo hizo kwa sasa hazitumiwi tena na wanajamii walio wengi. Katika jamii ya sasa ya Wapemba haiwi rahisi sana hasa vijana kutumia *ubinda* wanapokuwa katika kipindi cha

<sup>1</sup> Nguo inayovaliwa kwa kufungwa kiunoni na ncha zake kupitishwa baina ya mapaja na kuchomekwa kiunoni kwa nyuma BAKIZA (2012: 134).



hedhi. Mara nyingi wanatumia taulo za kike (*pedi*) au vitambaa maalumu. Vilevile, neno *ubinda* katika Kipemba kiasili lililikuwa na maana nyingine zaidi ya tulioyieleza hapa kuwa nguo inayovaliwa kwa kufungwa kiunoni na ncha zake kupitishwa baina ya mapaja na kuchomekwa kiunoni kwa nyuma (BAKIZA, 2012). Hali kadhalika, baadhi ya maneno chanzi yanayohusu mavazi katika Kipemba yametagusana na Kiswahili kwa hivyo, yamepokea mabadiliko kutoka Kiswahili sanifu. Mathalani, *dege* (*kaniki*), *nkuti* (*nsuli*), *nfyuo* (*suruali yenye kamba kiunoni*), *handawe*, *ulaiti* (*sanda*) na *kizoro* (*kilemba*). Maneno hayo katika Kiswahili sanifu na Kipemba kwa sasa yanajulikana kama *kaniki*, *msuli/nsuli*, *suruali ya kamba*, *chupi*, *sanda* na *kilemba*. Mabadiliko hayo ya maneno yanayohusu mavazi, yamesababishwa na mwingiliano wa lugha ya Kiswahili sanifu pamoja na kupotea kwa baadhi ya nguo ambazo zilikuwa zinatumiwa tangu kale na wanajamii hao. Hivyo, katika Nadharia ya Umuundo hayo ni mabadiliko ya kidiakronia ambayo yanasababishwa na mpito wa wakati. Aidha, tunaweza kuona tofauti ndogo ya sauti /m/ inayotumiwa katika Kiswahili sanifu na sauti /n/ inayotumiwa katika lahaja ya Kipemba. Hivyo, maneno *nsuli* (*msuli*) linaonekana kuathiriwa na Kiswahili ingawa limeendelea kuufuata muundo wa kifonolojia wa lahaja hii. Hata hivyo, tofauti hizo ndogondogo ni za kimataamshi tu hivyo, hazina athari kubwa hasa kwa lugha zenye asili moja.

#### **Mambo Yanayosababisha Kupotea kwa Maneno Chanzi na Athari zake**

Kuna sababu mbalimbali ambazo zimechangia kufifia kwa maneno chanzi katika lahaja ya Kipemba. Baadhi ya sababu zilizotajwa ni kama zifuatazo: Mosi, mwingiliano wa lugha: wakati jamii tofauti zinapokutana, maneno na muundo wa lugha unaweza kubadilishwa. Mabadiliko hayo yanaweza kutokea kwa njia ya kuingiza maneno mapya kutoka lugha nyingine. Katika utafiti huu, mwingiliano huo kwa kiasi kikubwa umesababishwa na elimu ya shule ambayo imewaathiri sana wazungumzaji wa lahaja ya Kipemba. Kupitia elimu wanayoipata baadhi ya wanajamii hawaoni fahari kuizungumza lahaja yao mbele ya kadamnasi ya watu. Aidha, wapo baadhi ya watu hasa vijana ambao wanaona hata aibu kuzungumza lahaja yao. Matokeo yake ni kuwa wanaegemea zaidi katika usanifu wa lugha kuliko lahaja. Kama ambavyo alisimulia mtoataarifa mmoja:

*...vijana wa sasa hawayeyebu maneno ya kale wajitia uzungu kwa kuwa wende sukuli. Siye hetwesoma sukuli, wavyele wetu wepinga kutufisa sukuli wakisema tutafuzwa ukafiri. Leo twayaona ndiyo hayo, hujui ntu nke wala ntu muume. Watu wake wasuka na watu waume vivyo. Watu waume wavaa suruali na watu wake pya huwabagui. Balaa liingili kyamboni ela si dogo! Tumuchile Mwenyezi Muungu tu, ela ni ntihani...*

*...vijana wa sasa hawayataki maneno ya kale wanajifanya wazungu kwa kuwa wamesoma shule. Sisi hatukusoma, wazee wetu walikataa kutupeleka shule walisema tutafundishwa ukafiri. Leo tunayaona, humjui mwanamke wala mwanaume. Wanawake wanasuka na wanaume pia. Wanaume wanavaa suruali na wanawake wote huwabagui. Balaa imeingia kijijini wala sio dogo! Tumumbeni Mwenyezi Muungu tu lakini ni mtihani... (Tafsiri yangu).*

Dokezo hilo la mtoataarifa huyo linatoa ithibati tosha kwamba maneno chanzi ya Kipemba yameanza kupotea hasa kwa vijana ambao wameathiriwa na elimu ya shuleni. Vijana ambao wanategemewa zaidi katika jamii kuwa na familia ambayo itarithishwa lahaja hii na utamaduni wake kwa vizazi vijavyo. Chambelecho Waswahili kuwa, *uivao ndiyo uvunwao*. Msemo huu una maana kwamba wazee wanategemewa kuondoka duniani mapema zaidi kuliko vijana. Kwa mnasaba huo, athari inayoweza kutokea ni kwamba, endapo wazee watatungulia mbele ya haki (watafariki) ni dhahiri kwamba maneno ya asili katika lahaja hii yatazidi kupotea hasa kwa vizazi vijavyo.



Pili, maingiliano ya lugha kutokana na uhamaji: makutano haya yanasababishwa na hamahama ya watu kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa ajili ya kutafuta maisha bora zaidi: hili nalo ni jambo mojawapo ambalo linachangia upotevu wa maneno chanzi. Jambo hili limetajwa na kuelezwa katika utafiti huu kwamba Wapemba wana tabia ya kuhama na kwenda maeneo mengine kutafuta maisha bora. Kwa hivyo, wanapohama katika maeneo yao ya asili na kujongea katika maeneo mengine, huwa wanatagusano na jamii nyingine zinazozungumza lugha mbalimbali. Hali hii ya kuhamahama ni sababu moja kuu inayochangia kupotea kwa maneno chanzi katika jamii. Juma (2019) anaeleza kwamba suala hili la kuhamahama si geni katika jamii nyingi za Afrika Mshariki. Uhamaji umekuwa kama sehemu ya maisha ya binadamu hapa ulimwenguni kwa sababu binadamu tumeumbwa na tamaa ya kutoridhika na tulivyo navyo. Hii ndiyo kawaida ya maisha ya binadamu. Mara nyingi watu huhama kufuata maisha mazuri ambayo wanadhani wameyakosa katika eneo lao na wanaamini wanaweza kuyapata katika eneo jingine. Hivyo, athari ya mchakato huu, unasababisha maneno chanzi katika lahaja hiyo kuingiliana na lugha zingine mbalimbali wanazokutana nazo.

Tatu, sababu nyingine ya kupotea kwa maneno chanzi ni kupotea kwa vifaa vya kiasili vilivyokuwa vinatumiwa katika jamiilugha ya Wapemba tangu kale. Kila jamii huwa inabadilika kutokana na mabadiliko mbalimbali ya kihistoria yanayotokea katika jamii hiyo. Katika lahaja ya Kipemba kuna vifaa mbalimbali vya kiasili ambavyo vimeshapitwa na wakati katika matumizi yake ya leo. Kwa mfano, maneno kama *dege (kaniki)*, *nfyuo (suruali yenye kamba kiunoni)* na *ubinda*. Nguo hizi katika jamii ya sasa ni nadra sana kuziona zikivaliwa katika jamii hiyo hasa kwa vijana. Hivyo, kwa kuwa nguo hizo kwa sasa hazionekani tena katika jamii ni dhahiri kwamba, hata hayo maneno yanayorejelea nguo hizo nayo yatapotea katika matumizi yake. Nguo hizo kwa sasa zinajulikana na kutumiwa na baadhi ya wazee wachache.

### **Mapendekezo na Hitimisho**

Katika utafiti huu tumegundua kuna maneno chanzi mbalimbali ambayo yameanza kupotea katika lahaja ya Kipemba, kiasi kwamba sio rahisi kwa vijana wa sasa kuweza kuyatumia katika mazungumzo yao. Hivyo, wanajamiilugha hasa vijana wanatakiwa kuzithamini, kujivunia, kuzitumia na kujifunza lahaja zao hasa kwa wazee ambao wanayafahamu maneno chanzi ya lahaja ya Kipemba. Aidha, wataalamu wa lugha ya Kiswahili na lahaja zake, wanafaa kufanya tafiti mbalimbali za kitaalamu kuhusu lahaja ya Kiswahili na utamaduni wake. Vilevile, vyombo vinavyohusika na uundaji wa istilahi za Kiswahili na lahaja zake vinatakiwa kuzihuisa na kisha kuzifuata hatua kadha wa kadha za uundaji istilahi zilizopendekezwa na wataalamu mbalimbali kama vile Mwansoko (1989), Massamba (1989), Sewangi (2007), Msigwa (2016) na Isindikiro (2023). Wataalamu hao wananasisitiza kwamba mchakato wa uundaji wa istilahi za Kiswahili uzipe kipaumbele lahaja za Kiswahili kabla ya lugha za Kibantu, lugha za Kiafrika na nyingine za kigeni.

### **Marejeleo**

- Anttila, R. (1972). *An Introduction to Historical and Comparative Linguistics*. Macmillan Publishing Co. Inc.
- Asiimwe, C. (2019). *Ulinganishi wa Lugha za "Runyačitara"*. [Tasnifu ya Uzamivu Haijachapiswa]. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- BAKIZA (2012). *Kamusi la Lahaja ya Kipemba*. Oxford University Press.
- Crystal, D. (2008). *A Dictionary of Linguistics and Phonetics*. Blackwell Publishing.
- Crystal, D. (2010). *Making Sense of Grammar*. Oxford University Press.
- De Saussure, F. (1916). *Course in General Linguistics*. McGraw-Hill.
- Harrison, D. (2007). *When Languages Die: The Extinction of the World's Languages and the Erosion of Human Knowledge*. Oxford University Press.



- Isindikiro, J. (2023). Mwachano wa Taratibu za Uundaji wa Istilahi za Kiswahili na Changamoto Zake katika Lugha: Mifano kutoka Istilahi za TATAKI na BAKITA. *Jarida la Mwanganga wa Lugha*, 8(1), 49-62.
- Juma, H. (2011). *Tofauti za Kiisimu baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili cha Wete katika Kisiwa cha Pemba*. [Tasnifu ya Umahiri Haijachapiswa]. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Juma, H. (2019). *Ulinganishi wa Kihistoria na Kiisimu wa Lahaja za Kiamu, Kimvoita, Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi*. [Tasnifu ya Uzamivu Haijachapiswa]. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Massamba, D. (1989). An Assessment of the Development and Modernization of The Kiswahili Language in Tanzania. *Language Adoption*, 60-78.
- Massamba, D. P. B. (2016). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. TUKI.
- Mekacha, R. (2011). *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili*. TUKI.
- Miller, R. (2021). Evaluating Local Multilingual Health Care Information Environments on the Internet: A Pilot Study. *International Journal of Environmental Research in Public Health*, 1-12.
- Msigwa, A. B. G. (2016). Changamoto za Istilahi katika Uandishi wa Tasnifu za Uzamili wa Tanzania. *Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*. 79.
- Mukumoto, J. (2019). *Language Change and Social Media: The Impact on African Languages*. Nairobi University Press.
- Mwansoko, H. (1989). The Principles, Methods and Procedures of Swahili Terminology Development in Tanzania: A Re-Examination of Basic Issues. *Journals of Asian and African Studies*, (38), 161-176.
- Ngugi wa Thiong'o. (1986). *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. East African Educational Publishers.
- TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. (Toleo la Tatu)*. Oxford University Press.
- Sewangi, S. (2007). Uundaji wa Istilahi za Kiswahili Kileksikografia na Athari zake. *Nordic Journal of African Studies*, 16 (3), 333-344.
- Ulfat, I. (2024). Nafasi ya Lugha za Kiasili katika Mchakato wa Kutoa Huduma za Matibabu: Mifano kutoka Tumbatu na Kojani, Visiwani Zanzibari. *Jarida la Mwanganga wa Lugha*, 9(1), 1-7.
- Valero-Garces, C. (2014). *Health, Communication and Multicultural Communities: Topics in Intercultural Healthcare Professionals*. Cambridge Scholars Publishing.